**TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI KWA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO MAPENDEKEZO YA MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA, MISHAHARA, VYANZO VYA NDANI NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18**

**Mhe. mwenyekiti**

Naomba kuwasilisha mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya Kawaida, Mishahara, Vyanzo vya ndani na Miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kabla ya kuwasilisha mapendekezo haya naomba kutoa mapitio ya Bajeti kwa mwaka 2015/16 na 2016/2017 hadi Desemba 2016.

**MAPITIO YA BAJETI KWA MWAKA 2015/16**

**Mh Mwenyekiti,** kwa mwaka wa fedha 2015/16 Halmashauri ilipanga kukusanya na kutumia kiasi Tsh **40,799,670,984** kwa mchanganuo ufuatao:-

| NA | CHANZO | MAKISIO(i) | MAPATO(ii) | MATUMIZI(iii) | %(iii/i) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Ndani | 1,893,854,500 | 540,823,755 | 454,990,115 | 24 |
| 2 | Miradi ya Maendeleo | 7,408,040,484 | 9,429,059,183 | 8,815,995,936 | 119 |
| 3 | Mishahara | 29,634,707,000 | 26,098,749,577 | 26,098,749,577 | 88 |
| 4 | Matumizi ya Kawaida | 1,863,069,000 | 2,537,855,550 | 2,537,855,550 | 136 |
| | **Jumla** | **40,799,670,984** | **38,606,488,065** | **37,907,591,178** | **92** |

**MAPITIO YA BAJETI KWA MWAKA 2016/17**

**Mhe. Mwenyekiti,** Mwaka wa fedha 2016/17, Halmashauri ya Wilaya Morogoro ilitegemea kukusanya na kutumia jumla Tsh **43,775,474,984** kwa mchanganuo ufuatao;

| NA | CHANZO | MAKISIO (i) | MAPATO (ii) | MATUMIZI (iii) | %(iii/ii) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Ndani | 1,960,554,500 | 987,756,626 | 525,671,322 | 53.2 |
| 2 | Miradi ya Maendeleo | 10,374,748,700 | 1,436,171,502 | 1,799,240,818 | 125 |
| 3 | Mishahara | 29,925,718,784 | 11,216,409,481 | 11,216,409,481 | 100 |
| 4 | Matumizi ya Kawaida | 1,514,453,000 | 483,312,363 | 483,312,363 | 100 |
| | **Jumla** | **43,775,474,984** | **14,123,649,972** | **14,024,633,984** | **99.29** |

**Mhe Mwenyekiti,`**

Kwa kipindi hiki cha miezi mitano , hali ya ukusanyaji mapato hasa ya vyanzo vya ndani siyo nzuri na hii imeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizopo kama zilivyoainishwa katika mpango .Hata hivyo Halmashauri iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kadiri tulivyopokea ruzuku ama kukusanya mapato yetu kwa lengo la kuboresha huduma kwa wananchi.

**SABABU ZA KUTOFIKIA MALENGO YA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI NA RUZUKU TOKA SERIKALI KUU.**

**A- MAPATO YA NDANI**

**Mhe. Mwenyekiti,**

i. Wakulima wadogo wadogo ambao wanalima kwa ajili ya chakula badala ya biashara. Hata wanaolima kwa biashara wanasingizia wanalima kwa ajili ya chakula (Mfano zao la mpunga) kwa kuwa uzalishaji wao uzidi magunia matano hivyo kuikosesha Halmashauri mapato.
ii. Kutokuwepo kwa vyama vya ukusanyaji mazao kama vile zao la ufuta, karafuu, pilipilimanga, mdalasini na mpunga ambavyo vingekusanya mazao kwa wakulima na kuwatafutia masoko ambapo Halmashauri ingepata ushuru kupitia vyama hivyo kama ilivyo kwa Mikoa ya kusini
iii. Kuwepo kwa njia nyingi zisizo rasmi (njia za panya) mfano Kiroka, Mlilingwa kwenda Kidugalo hadi Mdaula ambazo zinatumiwa na wafanyabiashara kutorosha mazao
iv. Wafanyabiashara wa viungo kutokubaliana na tozo ya asilimia 5

**B- KWA FEDHA ZA RUZUKU TOKA SERIKALI KUU**

Changamoto kubwa ni fedha za utekelezaji shughuli na miradi mbalimbali ya maaendeleo kutokufika kwa wakati na au miradi mingine kutopata fedha kabisa.

**JINSI YA KUTATUA CHANGAMOTO HIZO**

i. Menejimenti imeendelea kuimarisha kitengo cha Ushirika na masoko ili kuhamasisha vikundi viweze kuungana na kuunda vyama vya ushirika vitakavyosimamia kukusanya mazao na kutafuta masoko hatimaye Halmashauri ijipatie ushuru.
ii. Menejimenti imeanza utaratibu wa kuboresha timu ya usimamizi na ufuatiliaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kuimarisha vizuia vya ukaguzi na kutumia mfumo wa kieletronic (POS) kukusanyia mapato.
iii. Menejiment imeamua kuimarisha ushirikiano na vyombo vya Ulinzi na usalama ili kuthibiti mianya ya utoroshaji wa ushuru.

**MAPENDEKEZO YA BAJETI MWAKA 2017/2018**

**Mhe, Mwenyekiti,**

Baada ya kuonyesha hali halisi ya mapitio ya bajeti ya mwaka 2016/17 hadi Novemba 2016, naomba sasa kuwasilisha makisio ya bajeti ya mapato na matumizi ya kawaida, mishahara, mapato ya ndani na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2017/18.

**Mh Mwenyekiti,** Mapendekezo haya yamezingatia mambo muhimu yafuatayo;

i. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025
ii. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016-2021 (FYDP II )
iii. Mwongozo wa Bajeti wa mwaka 2016/17 na Sheria ya Bajeti Na 11 ya Mwaka 2015.
iv. Kuendelea kuunga mkono jitihada za Jamii zilizoanzishwa na zinazoendelea kwenye miradi ya maendeleo ngazi ya vijiji
v. Mpango Mkakati wa Halmashauri (2016 -2021)
vi. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015/2020
vii. Miongozo na sera mbalimbali za Kisekta
viii. Hotuba ya Mh Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bungeni Novemba 2015.

***Sudi Mpili***
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHURI YA WILAYA YA MOROGORO**